

## Neno la Jumamosi, 31. Mei 2014

---

Ndipo BWANA akamwambia Yakobo,  
“Rudi katika nchi ya baba zako na kwa watu wako,  
nami nitakuwa pamoja nawe.”

*Mwanzo 31,3*

Ndipo Yosefu akawaambia ndugu zake,  
“Mimi ninakaribia kufa.

Lakini kwa hakika Mungu atawasaidia  
na kuwachukueni kutoka nchi  
hii na kuwapeleka katika nchi  
aliyomwahidi kwa kiapo Abrahamu,  
Isaki na Yakobo.”

*Mwanzo 50,24*

---

The Lord said to Jacob,  
Return to the land of your fathers and to your kindred,  
and I will be with you.

*Genesis 31:3*

Joseph said to his brothers,  
I am about to die, but God will visit you  
and bring you up out of this land to the land  
that he swore to Abraham, to Isaac, and to Jacob.

*Genesis 50:24*

---

## Neno la Alhamisi, 29. Mei 2014

---

Yule mtu akaenda,  
akawaambia wale Wayahudi kuwa ni Yesu aliyemponya.

*Yohana 5,15*

Nimepewa mamlaka yote  
mbinguni na duniani. Kwa sababu hii,  
enendeni ulimwenguni mkawafanye  
mataifa yote kuwa wanafunzi,  
mkiwabatiza kwa Jina la Baba na la Mwana  
na la Roho Mtakatifu,  
nanyi wafundisheni kuyashika mambo  
yote niliyowaamuru ninyi.

*Mathayo 28,18-20*

---

The man went away and told the Jews  
that it was Jesus who had healed him.

*John 5:15 (ESV)*

*Jesus said:*

All authority in heaven and on earth has been given to me.  
Go therefore and make disciples of all nations,  
baptizing them in the name of the Father  
and of the Son and of the Holy Spirit,  
teaching them to observe all that I have commanded you.

*Matthew 28:18-20 (ESV)*

---

# Neno Mei 2014 The Word May 2014



Kiswahili Contemporary Version 2006  
English Standard Version

---



Project Bible 2.0 [www.bible2.net](http://www.bible2.net)

---

## Neno la Ijumaa, 2. Mei 2014

---

Niliamini, kwa hiyo nilisema,  
“Mimi nimeteseka sana.”

*Zaburi 116,10*

*Paulo akaandika:*

Twafurahi pia katika mateso,  
kwa sababu tunajua kuwa mateso huleta saburi,  
nayo saburi huleta uthabiti  
wa moyo na uthabiti wa moyo huleta tumaini.

*Warumi 5,3-4*

---

I believed, even when I spoke,  
“I am greatly afflicted”.

*Psalms 116:10*

*Paul writes:*

We rejoice in our sufferings,  
knowing that suffering produces endurance,  
and endurance produces character,  
and character produces hope.

*Romans 5:3-4 (ESV)*

---

---

### Neno la Jumanne, 27. Mei 2014

---

Tukisema kwamba twashirikiana  
naye huku tukienda gizani,  
wasema uongo, wala hatutendi lililo kweli.  
*1 Yohana 1,6*

BWANA Mungu wenu anawajaribu kuangalia kama  
mnampenda kwa  
moyo wenu wote na kwa roho yenu yote.  
*Kumbukumbu La Torati 13,3*

---

If we say we have fellowship with him  
while we walk in darkness,  
we lie and do not practice the truth.  
*1 John 1:6 (ESV)*

The Lord your God is testing you,  
to know whether you love the Lord your God  
with all your heart and with all your soul.  
*Deuteronomy 13:3 (ESV)*

---

### Neno la Jumapili, 25. Mei 2014

---

*Yesu awaambia Wayuda:*  
Mimi ni mkate wa uzima ule uliotoka mbinguni.  
Mtu ye yote akiula mkate huu, ataishi milele.  
*Yohana 6,51*

Akiisha kukamilishwa, akawa chanzo  
cha wokovu wa milele  
kwa wote wanaomtii.  
*Waebrania 5,9*

---

*Jesus said to the Jews:*  
I am the living bread that came down from heaven.  
If anyone eats of this bread, he will live forever.  
*John 6:51 (ESV)*

Being made perfect,  
Christ became the source of eternal salvation  
to all who obey him.  
*Hebrews 5:9 (ESV)*

---

### Neno la Jumapili, 4. Mei 2014

---

Kama uso wako hauendi pamoja nasi, usituondoe hapa.  
*Kutoka 33,15*

*Kristo asema:*  
Hakika Mimi niko pamoja nanyi sikuzote,  
hadi mwisho wa nyakati.  
*Mathayo 28,20*

---

If your presence will not go with me,  
do not bring us up from here.  
*Exodus 33:15 (ESV)*

*Christ says:*  
I am with you always, to the end of the age.  
*Matthew 28:20 (ESV)*

---

### Neno la Jumanne, 6. Mei 2014

---

Eliya akasimama mbele ya watu na kusema,  
“Mtasitasita katika mawazo mawili hadi lini?  
Ikiwa BWANA ndiye Mungu, mfuateni yeye,  
lakini ikiwa Baali ni Mungu, basi mfuateni yeye.”  
*1 Wafalme 18,21*

Je,  
ndugu zangu, mtini waweza kuzaa zeituni,  
au mzabibu kuzaa tini?  
Wala chemchemi ya maji ya chumvi  
haiwezi kutoa maji matamu.  
*Yakobo 3,12*

---

Elijah came near to all the people and said,  
How long will you go limping  
between two different opinions?  
If the Lord is God, follow him;  
but if Baal, then follow him.  
*1 Kings 18:21 (ESV)*

Can a fig tree, my brothers, bear olives,  
or a grapevine produce figs?  
Neither can a salt pond yield fresh water.  
*James 3:12 (ESV)*

### Neno la Ijumaa, 23. Mei 2014

---

Wamenionea mno tangu ujana wangu,  
lakini bado hawajanishinda.  
*Zaburi 129,2*

Twataabika kila upande, lakini hatuangamizwi,  
twaona wasiwasi lakini hatukati tamaa.  
*2 Wakorinto 4,8*

---

Greatly have they afflicted me from my youth,  
yet they have not prevailed against me.  
*Psalm 129:2 (ESV)*

We are afflicted in every way, but not crushed;  
perplexed, but not driven to despair.  
*2 Corinthians 4:8 (ESV)*

### Neno la Alhamisi, 8. Mei 2014

---

BWANA humfanya mtu maskini naye hutajirisha,  
hushusha na hukweza.  
Humwinua maskini kutoka mavumbini  
na humwinua mhitaji kutoka lundo la majivu.  
*1 Samweli 2,7-8*

Mungu ndiye ahukumuye:  
Humshusha huyu na kumkweza mwingine.  
*Zaburi 75,7*

---

The Lord makes poor and makes rich;  
he brings low and he exalts.  
He raises up the poor from the dust;  
he lifts the needy from the ash heap.  
*1 Samuel 2:7-8 (ESV)*

It is God who executes judgment,  
putting down one and lifting up another.  
*Psalm 75:7 (ESV)*

### Neno la Jumatano, 21. Mei 2014

---

Kwa kuwa BWANA Mungu wenu ni moto ulao,  
Mungu mwenye wivu.  
*Kumbukumbu La Torati 4,24*

Hakuna kiumbe cho chote kilichofichika  
machoni pa Mungu. Kila  
kitu kimefunuliwa na kiko wazi machoni pake  
Yeye ambaye Kwake tutatoa hesabu.  
*Waebrania 4,13*

---

The Lord your God is a consuming fire, a jealous God.  
*Deuteronomy 4:24 (ESV)*

No creature is hidden from his sight,  
but all are naked and exposed to the eyes of him  
to whom we must give account.  
*Hebrews 4:13 (ESV)*

### Neno la Jumamosi, 10. Mei 2014

---

Tunafurahi katika Mungu kwa  
njia ya Bwana wetu Yesu Kristo,  
ambaye kwa kupitia Kwake tumepata upatanisho.  
*Warumi 5,11*

akiisha kuifuta ile hati yenye  
mashtaka yaliyokuwa yanatukabili pamoja na amri zake,  
aliiondoa isiwepo tena,  
akiigongomea kwenye msalaba Wake.  
*Wakolosai 2,14*

---

We rejoice in God through our Lord Jesus Christ,  
through whom we have now received reconciliation.  
*Romans 5:11 (ESV)*

God cancelled the record of debt  
that stood against us with its legal demands.  
This he set aside, nailing it to the cross.  
*Colossians 2:14 (ESV)*

---

## Neno la Jumatatu, 19. Mei 2014

---

*Musa aimba juu ya Yakobu, watu wa Mungu:*

Alimhifadhi na kumtunza,  
akamlinda kama mboni ya jicho lake.  
Kama tai avurugaye kiota chake  
na kurukaruka juu ya makinda yake,  
ambaye hutanda mabawa yake  
na kuwadaka na kuwachukua kwenye mbawa zake.  
*Kumbukumbu La Torati 32,10-11*

BWANA asema, "Nimewapenda ninyi."  
*Malaki 1,2*

---

*Mose sings about Jacob, the Lord's people:*

He kept him as the apple of his eye.  
Like an eagle that stirs up its nest,  
that flutters over its young,  
spreading out its wings, catching them,  
bearing them on its pinions.  
*Deuteronomy 32:10-11 (ESV)*

I have loved you, says the Lord.  
*Malachi 1:2*

---

---

## Neno la Jumamosi, 17. Mei 2014

---

Hakuna mtumishi awezaye kuwatumikia mabwana wawili.  
Ama atamchukia mmoja na kumpenda  
mwingine au atamheshimu mmoja na kumdharau mwingine.  
Hamwezi kumtumikia Mungu pamoja na mali.  
*Luka 16,13*

Msiupende ulimwengu wala mambo yaliyoko ulimwenguni.  
Kama mtu ye yote akiupenda ulimwengu,  
kumpenda Baba hakumo ndani yake.  
*1 Yohana 2,15*

---

No servant can serve two masters,  
for either he will hate the one and love the other,  
or he will be devoted to the one and despise the other.  
You cannot serve God and money.  
*Luke 16:13*

Do not love the world or the things in the world.  
If anyone loves the world,  
the love of the Father is not in him.  
*1 John 2:15 (ESV)*

---

---

## Neno la Jumatatu, 12. Mei 2014

---

Msiwe na wasiwasi kuhusu maisha yenu:  
mtakula nini au mtakunywa nini,  
au kuhusu miili yenu, mtavaa nini.  
Je, maisha si zaidi ya chakula na mwili zaidi ya mavazi?  
*Mathayo 6,25*

Wakati wasiwasi ulipokuwa mwingi ndani yangu,  
faraja yako ilinipa furaha nafsini mwangu.  
*Zaburi 94,19*

---

Do not be anxious about your life,  
what you will eat or what you will drink,  
nor about your body, what you will put on.  
Is not life more than food,  
and the body more than clothing?  
*Matthew 6:25 (ESV)*

When the cares of my heart are many,  
your consolations cheer my soul.  
*Psalms 94:19*

---

---

## Neno la Jumatano, 14. Mei 2014

---

BWANA, ambaye ni mwema na amsamehe  
kila mmoja ambaye anauelekeza moyo wake kumtafuta  
Mungu.  
*2 Mambo ya Nyakati 30,18-19*

Toka mbinguni Bwana anawachungulia  
wanadamu chini aone kama wako wenye akili,  
wo wote wanaomtafuta Mungu.  
*Zaburi 14,2*

---

May the good Lord pardon everyone  
who sets his heart to seek God, the Lord,  
the God of his fathers.  
*2 Chronicles 30:18-19 (ESV)*

The Lord looks down from heaven on the children of man,  
to see if there are any who understand,  
who seek after God.  
*Psalms 14:2 (ESV)*

---

---

### Neno la Alhamisi, 1. Mei 2014

---

Walipomlilia BWANA katika shida yao,  
naye akawaokoa kutoka kwenye taabu yao.  
*Zaburi 107,13*

Msihuzunike, kwa kuwa furaha ya BWANA ni nguvu zenu.  
*Nehemia 8,10*

---

They cried to the Lord in their trouble,  
and he delivered them from their distress.  
*Psalms 107:13 (ESV)*

Do not be grieved,  
for the joy of the Lord is your strength.  
*Nehemiah 8:10 (ESV)*

---

Scriptures taken from Kiswahili Contemporary Version  
Copyright (c) 1984, 1989, 2006 by International Bible Society(R)  
Used by permission. All rights reserved worldwide.



---

### Neno la Ijumaa, 30. Mei 2014

---

jiosheni na mkajitakase.  
Yaondoeni matendo yenu maovu mbele zangu!  
Acheni kutenda mabaya,  
*Isaya 1,16*

Wana heri walio na moyo safi,  
maana hao watamwona Mungu.  
*Mathayo 5,8*

---

Wash yourselves; make yourselves clean;  
remove the evil of your deeds from before my eyes;  
cease to do evil.  
*Isaiah 1:16*

Blessed are the pure in heart,  
for they shall see God.  
*Matthew 5:8 (ESV)*

---

---

### Neno la Jumamosi, 3. Mei 2014

---

Katika hili mnafurahi sana,  
ingawa sasa kwa kitambo kidogo,  
ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa  
kwa majaribu ya namna nyingi.  
*1 Petro 1,6*

Ndugu zangu, hesabuni kuwa ni furaha tupu  
mnapopatwa na majaribu mbalimbali.  
*Yakobo 1,2*

---

In this you rejoice,  
though now for a little while, if necessary,  
you have been grieved by various trials.  
*1 Peter 1:6 (ESV)*

Count it all joy, my brothers,  
when you meet trials of various kinds.  
*James 1:2 (ESV)*

---

---

### Neno la Jumatano, 28. Mei 2014

---

Ninyi ni nuru ya ulimwengu.  
*Mathayo 5,14*

*Paulo akaandika:*

Fanyeni mambo yote bila kunung'unika wala kushindana,  
ili msiwe na lawama wala hatia,  
bali mwe wana wa Mungu wasio  
na kasoro katika kizazi chenye ukaidi na kilichopotoka,  
ambacho ndani yake ninyi  
mnang'aa kama mianga ulimwenguni.  
*Wafilipi 2,14-15*

---

You are the light of the world.  
*Matthew 5:14 (ESV)*

*Paul writes:*

Do all things without grumbling or questioning,  
that you may be blameless and innocent,  
children of God without blemish  
in the midst of a crooked and twisted generation,  
among whom you shine as lights in the world.  
*Philippians 2:14-15 (ESV)*

---

## Neno la Jumatatu, 5. Mei 2014

---

Shangilieni pamoja na Yerusalemu  
na mfurahi kwa ajili yake,  
ninyi nyote mnaompenda,  
shangilieni kwa nguvu pamoja naye,  
ninyi nyote mnaomboleza juu yake.  
*Isaya 66,10*

*Paulo akandika:*

Si kwamba tunatawala imani yenu,  
bali twatenda kazi pamoja nanyi kwa ajili ya furaha yenu,  
kwa sababu ni kwa imani mwasimama imara.  
*2 Wakorinto 1,24*

---

Rejoice with Jerusalem, and be glad for her,  
all you who love her;  
rejoice with her in joy,  
all you who mourn over her.  
*Isaiah 66:10 (ESV)*

*Paul writes:*

Not that we lord it over your faith,  
but we work with you for your joy,  
for you stand firm in your faith.  
*2 Corinthians 1:24 (ESV)*

---

## Neno la Jumatano, 7. Mei 2014

---

Mtanitii mimi, nami nitakuwa Mungu wenu  
nanyi mtakuwa watu wangu.  
*Yeremia 7,23*

BWANA ni mwenye haki,  
hata hivyo niliasi dhidi ya amri yake.  
*Maombolezo 1,18*

---

Obey my voice, and I will be your God,  
and you shall be my people.  
*Jeremiah 7:23 (ESV)*

The Lord is in the right,  
for I have rebelled against his word.  
*Lamentations 1:18 (ESV)*

---

## Neno la Jumatatu, 26. Mei 2014

---

Namlilia Mungu Aliye Juu Sana,  
Mungu atimizaye makusudi yake kwangu.  
*Zaburi 57,2*

Tazama, mambo ya kwanza yametokea,  
nami natangaza mambo mapya,  
kabla hayajatokea nawatangazia habari zake.  
*Isaya 42,9*

---

I cry out to God Most High,  
to God who fulfills his purpose for me.  
*Psalms 57:2 (ESV)*

Behold, the former things have come to pass,  
and new things I now declare;  
before they spring forth I tell you of them.  
*Isaiah 42:9 (ESV)*

---

## Neno la Jumamosi, 24. Mei 2014

---

Hapa hatuna mji udumuo, bali tunautafuta ule ujao.  
*Waebrania 13,14*

*Yohana aandika kuhusu mji mtakatifu:*  
Mataifa yatatembea yakiangaziwa  
na nuru yake na wafalme wa  
duniani wataleta fahari yao ndani yake.  
*Ufunuo wa Yohana 21,24*

---

Here we have no lasting city,  
but we seek the city that is to come.  
*Hebrews 13:14 (ESV)*

*John describes the heavenly city:*  
By its light will the nations walk,  
and the kings of the earth will bring their glory into it.  
*Revelation 21:24 (ESV)*

---

---

### Neno la Ijumaa, 9. Mei 2014

---

Ole wao manabii wapumbavu wafuatao  
roho yao wenyewe na wala hawajaona cho chote!  
*Ezekieli 13,3*

Lakini sasa inuka usimame,  
kwa miguu yako, kwa sababu nimekutokea kwa  
kusudi hili ili kukuweka utumike  
na kushuhudia juu ya mambo  
ambayo umeyaona na yale nitakayokutokea kwayo.  
*Matendo ya Mitume 26,16*

---

Woe to the foolish prophets  
who follow their own spirit,  
and have seen nothing!  
*Ezekiel 13:3 (ESV)*

*The Lord said to Paul:*

I have appeared to you for this purpose,  
to appoint you as a servant and witness  
to the things in which you have seen me  
and to those in which I will appear to you.  
*Acts 26:16 (ESV)*

---

### Neno la Jumapili, 11. Mei 2014

---

Watakapowapeleka humo,  
msisumbuke kufikirifikiri mtakalosema,  
kwa maana mtapewa la kusema wakati huo.  
*Mathayo 10,19*

*Petro na Yohana wajibu viongozi wa Kiyahudi:*  
Lakini sisi hatuwezi kuacha kusema  
yale tuliyoyaona na kuyasikia.  
*Matendo ya Mitume 4,20*

---

When they deliver you over,  
do not be anxious  
how you are to speak or what you are to say,  
for what you are to say will be given to you in that hour.  
*Matthew 10:19 (ESV)*

We cannot but speak of what we have seen and heard.  
*Acts 4:20 (ESV)*

---

### Neno la Alhamisi, 22. Mei 2014

---

Lakini kwako kuna msamaha, kwa hiyo wewe unaogopwa.  
*Zaburi 130,4*

Ingawa dhambi zenu ni kama rangi nyekundu  
zitakuwa nyeupe kama theluji, ingawa ni nyekundu  
sana kama damu, zitakuwa nyeupe kama sufu.  
*Isaya 1,18*

---

With you there is forgiveness,  
that you may be feared.  
*Psalms 130:4 (ESV)*

Though your sins are like scarlet,  
they shall be as white as snow;  
though they are red like crimson,  
they shall become like wool.  
*Isaiah 1:18*

---

### Neno la Jumanne, 20. Mei 2014

---

Ndipo Mungu akamwambia Noa na wanawe pamoja naye:  
Sasa mimi ninaweka agano langu nanyi,  
pamoja na uzao wenu baada yenu,  
pia na kila kiumbe hai kilichokuwa pamoja nanyi  
na kila kiumbe hai duniani.  
*Mwanzo 9,8-10*

Milima na vilima viondolewe,  
hata hivyo upendo wangu usiokoma  
kwenu hautatikisika wala agano  
langu la amani halitaondolewa,  
asema BWANA, mwenye huruma juu yenu.  
*Isaya 54,10*

---

God said to Noah and to his sons with him,  
Behold, I establish my covenant with you  
and your offspring after you,  
and with every living creature that is with you.  
*Genesis 9:8-10 (ESV)*

The mountains may depart and the hills be removed,  
but my steadfast love shall not depart from you,  
and my covenant of peace shall not be removed,  
says the Lord, who has compassion on you.  
*Isaiah 54:10 (ESV)*

---

## Neno la Jumanne, 13. Mei 2014

---

*Yesu akasema:*

Ye yote anionaye Mimi, amemwona Yeye aliyenituma.

*Yohana 12,45*

Yeye ni mfano wa Mungu asiyeonekana,  
mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.

*Wakolosai 1,15*

---

*Jesus cried out and said:*

Whoever sees me sees him who sent me.

*John 12:45 (ESV)*

Jesus is the image of the invisible God,  
the firstborn of all creation.

*Colossians 1:15*

---

---

## Neno la Alhamisi, 15. Mei 2014

---

Wakati wa uzee watakuwa bado wanazaa matunda,  
watakuwa wabichi na wamejaa nguvu, wakitangaza,  
“BWANA ni mkamilifu,  
Yeye ni Mwamba wangu na hamna uovu ndani yake.”

*Zaburi 92,14-15*

Ee Bwana, ulichukua shauri langu,  
ukaukomboa uhai wangu.

*Maombolezo 3,58*

---

They still bear fruit in old age;  
they are ever full of sap and green,  
to declare that the Lord is upright;  
he is my rock, and there is no unrighteousness in him.

*Psalms 92:14-15 (ESV)*

You have taken up my cause, O Lord;  
you have redeemed my life.

*Lamentations 3:58*

---

---

## Neno la Jumapili, 18. Mei 2014

---

Wakumbukeni viongozi wenu,  
wale waliowaambia neno la Mungu.  
Angalieni matokeo ya mwenendo  
wa maisha yao mkaiige imani yao.

*Waebrania 13,7*

Endeleeni kukaa ndani Yake. Mwe na mizizi,  
mkiwa mmejengwa ndani Yake, mkiimarishwa katika  
imani kama mlivyofundishwa  
na kufurika kwa wingi wa shukrani.

*Wakolosai 2,6-7*

---

Remember your leaders,  
those who spoke to you the word of God.  
Consider the outcome of their way of life,  
and imitate their faith.

*Hebrews 13:7*

Walk in Christ Jesus, rooted and built up in him  
and established in the faith, just as you were taught,  
abounding in thanksgiving.

*Colossians 2:6-7 (ESV)*

---

---

## Neno la Ijumaa, 16. Mei 2014

---

Ufalme wa Mungu umefanana na punje ya haradali  
ambayo ni ndogo sana, ambayo mtu aliichukua na  
kuipanda katika shamba lake. Nayo ikakua, ikawa mti  
na ndege wa angani wakatengeneza  
viota vyao kwenye matawi yake.

*Luka 13,19*

Kwa sababu kwa dhabihu moja  
amewafanya kuwa wakamilifu milele wale wote  
wanaotakaswa.

*Waebrania 10,14*

---

The kingdom of God is like a grain of mustard seed  
that a man took and sowed in his garden,  
and it grew and became a tree,  
and the birds of the air made nests in its branches.

*Luke 13:19 (ESV)*

By a single offering Jesus Christ has perfected for all time  
those who are being sanctified.

*Hebrews 10:14 (ESV)*

---